*SWAHILI FORUM 15 (2008): 73-94*

# MABADILIKO KATIKA UMBO LA USHAIRI NA ATHARI ZAKE KATIKA USHAIRI WA KISWAHILI

FLORENCE NGESA INDEDE

## 1. Utangulizi

Mwanadamu amejaribu kwa vyovyote vile kuvumbua na kunyumbua mambo mapya ambayo yataleta mvuto na kupimia akili yake kiubunifu katika hali ya kutaka kutangamana zaidi na binadamu mwenzake au kutaka kuelewa zaidi ulimwengu wake. Ndiposa washairi wengi wa kisasa wanashikilia kwamba ulimwengu unabadilika na hivyo utamaduni wa ushairi lazima ubadilike pia asemavyo Mazrui (1988:viii):

> ...utamaduni hauna budi kubadilika maadamu uchumi na siasa za nchi zaendelea kubadilika.

Mwelekeo huo unasisitizwa katika mjadala wa Wangari Mwai (1988:5) anayeonyesha kuwa washairi wa kisasa wanaeleza kwamba fasihi hubadilika katika umbo na maudhui na kwa hivyo ushairi wa Kiswahili sharti uruhusu mabadiliko yanayotokea katika ushairi huru.

Katika utangulizi wa swala la “Ushairi, Lugha na Mawazo” (“Poetry, Language and Thought”) Martin Heidegger (1971:xi) anazua swala la tofauti iliyopo kati ya mfikiriaji mshairi na mshairi mfikiriaji; kwamba ili kuwa mshairi mkomavu kuna ufikiriaji ambao mshairi lazima akamilishe. Ufikiriaji ulio na usafi, uzito na umoja wa ushairi. Uwazaji wa kiwango hiki huongezea ubora na utaalamu wa lugha ya ushairi. Fikra kama hizi si za kiajali bali zinakwenda sambamba na ukuaji wa maono ya washairi kwani mshairi alazimika kuzungumzia maudhui ya kiungu, bahari, mawingu, milima, maovu, maafa n.k. Hiki ni kiwango cha juu cha ufikiriaji na uwazaji unaozungumzia mambo ya kidhahania kuwasilisha uhalisia.

Kwa kuzingatia wazo hilo la Martin Heidegger tunatambua kwamba wazalendo katika nchi huru za Afrika wamekumbana na uhalisia wa kutaka kuimarisha maendeleo baada ya kutambua udhaifu wa mataifa changa ya Kiafrika kwa kubakia nyuma katika nyanja mbalimbali, za siasa, uchumi, utamaduni au ujamii. Kwa kutafuta suluhisho kwa matatizo haya watu binafsi, vikundi na wananchi mbalimbali wamechukua mielekeo tofauti katika kuhamasisha au kuchochea mabadiliko. Katika harakati hizi, mabadiliko mengine yamekuwa kwa mwendo wa pole na mengine mwendo wa kasi. Asasa za kijamii zikiwemo fasihi – ushairi zimeathirika katika harakati hizi za ama kuhifadhi ya kale au kuyatupilia mbali na kuvumbua mapya zaidi kuchukua nafasi hizi.

Jambo la kutilia maanani ni kwamba ilivyo katika mataifa mengine yaliyokuwa chini ya koloni mbalimbali za kigeni, kulitokea matukio mbalimbali yaliyokumbanisha washairi wa kipindi hiki na kuwafikirisha zaidi katika kuibuka na mitindo mipya. Utawala awali ulikutanisha mataifa ya Kiafrika moja kwa moja na mataifa ya kigeni, usambazaji wa elimu mpya, maono na uchangamano wa fikra kiasi cha washairi kuanza kusikitikia hali ya maisha

yao ya leo na ya keshoe. Ni dhahiri kwamba wengi walisikitikia hali ya mataifa haya kuendelea kubaki nyuma kimaendeleo na hasa kifasihi na hivyo kuzua hamu ya kusasanisha nchi zao, fasihi na utamaduni kwa kuiga mielekeo ya ustaarabu wa mataifa ya ama magharibi au mashariki. Ndiposa tunapata kwamba mielekeo ya kifasihi ya kipindi baada ya uhuru ilivunja umbo la kitamaduni na kufanyia mjarabu maumbo mapya ya ushairi. Kufuatia ushairi wa Kezilahabi katika “Kichomi” (1974) na uchochezi wake kwenye dibaji ya diwani hii washairi wa baadaye waliamua kutofuata kanuni za Amri Abedi katika “Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri” (1954). Lengo hasa lilikuwa kuleta mapinduzi katika umbo, miundo na mitindo katika ushairi kwa minajili ya kuepukana na uchovu uliotokana na mtindo ule ule wa kurarisha vina na mizani. Wana-usasa walionelea kuwa ushairi wa awali haufikii uma wa kawaida kwa sababu za matumizi ya lugha ngumu ya kimafumbo, methali na taswira ambazo si rahisi kufasirika. Ni kana kwamba waliutoa ushairi “chuoni hadi sokoni”.

Utangamano katika mifumo mbalimbali ya kielimu ni shughuli ambayo imechangia sana mabadiliko haya ya umbo la ushairi ingawaje tunapata kuwa washairi wa kijadi na wa kisasa wote wanashutumiana kuwa mabadiliko haya yanatokana na athari za nje. Ni kweli kwamba utangamano kati ya wasomi wa Kiafrika na watu wa mataifa mbalimbali ikiwemo Marikani, Uingereza, Ujerumani, Urusi, Uarabu, Uhindi umeandaa mawazo, fikra, mazingira na mawanda mageni katika fani hii. Uhusiano huu umeimarisha na kuchochea hisia za uzalendo miongoni mwa watunzi na wahakiki na hapo hapo kueneza na kusambaza hisia za ujamii. Si muhali kutambua kwamba ni kutokana na changamoto na utangamano huu wa kilimwengu ndiposa washairi huru wakaamua kubadlisha miundo na mitindo ya mitazamo ya kifasihi asemavyo Mazrui (1988:ix);

> ...ilhamu ya washairi hawa wapya imeamshwa na hali nyingine tu ya mazingira, kwamba mdundo wa ilhamu yao unatokana na ngoma nyingine, kwamba katika maisha yao wamekumbana na bahari nyingine za ufasaha ambazo mawimbi yake yamepelekea kumudu mbinu nyingine za unahodha wa fasihi.

Katika wasilisho hili tunajadili mabadiliko haya ya kimaumbo na athari zake katika ushairi wa Kiswahili. Si lengo letu kushawishi msomaji kujiunga na kikundi fulani cha ushairi bali kuangazia hoja mwafaka zinazotokana na mivutano na mikinzano katika mabadiliko haya, na namna mitazamo hii inavyofanikisha maendeleo ya ushairi.

## 2. Taswira ya umbo awali na umbo la kisasa

Wanakipindi cha urasimi mkongwe na urasimi mpya walienzi sana umbo la shairi lililoasisiwa na Muyaka bin Haji[1] Shaaban Robert, Mathias Mnyampala, Mwalimu Hassan Mbega n.k walidumisha na kuendeleza umbo hili kiasi cha kwamba yeyote ambaye angeulizwa juu ya ufafanuzi wa ushairi wa Kiswahili angeeleza kuwa ushairi wa Kiswahili ni tarbia )[2] na una umbo lifuatalo:

---------------------------- 8a -------------------------------8b
---------------------------- 8a -------------------------------8b
---------------------------- 8a -------------------------------8b
---------------------------- 8b--------------------------------8x

Yaani mishororo minne katika kila ubeti, mizani 8 katika kila kipande na urari wa kina cha kati na kina cha mwisho. Kina cha mshororo wa nne hubadilishana nafasi ambapo kile cha mwisho huja kati na cha kati huja mwisho au mshairi aamue kuzua kina kingine ilivyoonyeshwa katika muundo huo. Utawala na uzoefu wa umbo hili uliwafanya wahakiki, watafiti, wanafalsafa wa kifasihi na wasomi wengineo kufikiria kwamba ushairi wa Kiswahili haubadiliki na hivyo haukui. Hadi wa leo unapomuuliza mwanafunzi wa shule ya msingi na sekondari nchini Kenya swali la je ushairi ni kitu gani, atakujibu kwa kuelezea vipengee vya umbo hili la tarbia.

Kuambatana na misingi ya kanuni za ushairi mkongwe maoni mbalimbali yametolewa juu ya kijelezi cha ushairi ambapo wanamapokeo wamesisitiza uwepo wa urari wa vina na ulinganinfu wa mizani katika kila ubeti. Kwa mfano Shaaban Robert (Massamba 1983:55) asema:

> Ushairi ni sanaa ya vina inayopambanuliwa kama nyimbo, mashairi na tenzi. Zaidi ya kuwa sanaa ya vina, ushairi una ufasaha wa maneno machache au muhtasari. Mwauliza wimbo, shairi na tenzi ni nini? Wimbo ni shairi ndogo, ushairi ni wimbo mkubwa na utenzi ni upeo wa ushairi. Mwauliza tena kina na ufasaha huweza kuwa nini? Kina ni mlingano wa sauti za herufi. Kwa maneno mengine huitwa mizani ya sauti, na ufasaha ni uzuri wa lugha. Mawazo maono na fikra za ndani zinapoelezwa kwa muhtasari wa shairi huvuta moyo kwa namna ya ajabu.

Abdilatif Abdalla (Massamba 1983:57) naye akasema kwamba:

> ... Utungo ufaao kupewa jina la ushairi si utungo wowote bali ni utungo ambao katika kila ubeti wake kuna ulinganifu wa vina vitukufu vilivyopangwa kimoja baada ya chenziye, wenye vipande vilivyo na ulinganifu wa mizani zisizo pungufu wala zilizo zaidi. Na vipande hivyo viwe vimetandwa na maneno ya mkato maalum na yenye lugha nyoofu, tamu na laini. Lugha ambayo ina uzito wa fikra, tamu kwa mdomo wa kusema, tumbuizi kwa masikio ya kuusikia na yenye kuathiri moyo uliokusudiwa na kama ilivyokusudiwa.

[1] Wataalamu wa uhakiki wa ushairi wakiwemo Kingei na Kemoli (2001:19), na Wangari Mwai (1988:44) wanaelezea kwamba utungo wa unne au tarbia ulizuka karne ya 18 hasa katika utunzi wa Mashairi ya Muyaka.

[2] Njogu na Chimerah (1999:100) wanaeleza kuwa utungo ukiwa na mishororo minne huitwa tarbia na ukiwa na mishororo mitano huitwa takhmisa. Pia Kingei na Kemoli (2001:18) wanafasili tarbia kuwa shairi lililo na mishororo minne katika beti zake, pia huitwa unne.

Mayoka (1984:3) atoa maelezo yake kwa kusema:

> Ushairi ni mtungo wa kisanaa ulio na mpangilio maalum na lugha ya mkato ambayo ndani yake ina vina, urari wa mizani na muwala maalum ambavyo kwa pamoja huwa na fani na maudhui yahusuyo hisi fulani au tukio juu ya maisha ya mtu au watu wa mazingira na wakati maalum.

Kulingana na fasili hizi shairi ambalo ni la kutolewa mfano ni "Mcheza kwao hutunzwa" (Wallah 1988:154):

Kulla aliye mwele*wa*, aghalabu hupongez*wa*
Hupongezwa na kupa*wa*, tunu bora ya kutuz*wa*
Kutuzwa na kuambi*wa*, wanasi wamependez*wa*
Mcheza kwao hutuz*wa*, au la kushangil*ia*

Kijumla shairi hili lina beti saba. Ni tarbia ambayo ina mishororo minne katika kila ubeti, kina cha kati ni *wa* na cha mwisho ni *zwa* hivyo linachukua muundo ufuatao:

-8a -8b
-8a -8b
-8a -8b
-8a -8b

} Kina katika mshororo wa nne kinabadilika hivi kwamba kile cha nje katika mishororo ya awali kinakuja kati na cha kati kinakuja mwisho

Katika kukuza na kuzua mitindo na maumbo mapya wanamapokeo wanatumia miundo tofauti ya kina kama katika mifano ifuatayo;

-8a -8b
-8a -8b
-8a -8b
-8a -8b

} Katika hali hii kina cha mshororo wa nne hakibadiliki

-8a -8b
-8a -8b
-8c -8d
-8c -8d
-8e -8f
-8e -8f

} Katika tasdisa (Kuvuna, Mvati na Maliachi 1992:13)[3],mshairi anaweza kuzua kina tofauti cha kati na cha mwisho baada ya mishororo miwili

Mtindo umekuwa na taratibu hizi hata katika tathlitha (Kitula na Kemoli 2001:17) ambapo tuna muundo huu;

| | |
|---|---|
| Nakupa wa*sia*, moyo shika m*no* | 6a -6b |
| Niloyakimb*iy*a, henda penye so*no* | -6a -6b |
| Yangakujil*iya*, usinene ne*no* | -6a -6b |

Mbali na tathlitha yenye vipande viwili kuna pia yenye vipande vitatu katika kila mshororo wenye mizani –8 –8 –8. Katika historia ya tenzi tumekumbana na umbo la mgao wa 4

---

[3] Kuvuna, Mvati na Maliachi (1992:13) wanafasiri tasdisa kuwa ni bahari ya mishororo sita katika kila ubeti.

mishororo ya mizani nane kwa nane kama katika Utenzi wa Mwana Kupona, Utenzi wa Uhuru n.k. Kijumla tunapata ya kuwa umbo la ushairi husika limeweza kuainisha ushairi huo katika bahari maalum kwa mfano tathlitha, tarbia, takhimisa, utenzi[4], inkishafi n.k.

Tulivyodokeza katika utangulizi, vikundi mbalimbali vya wataalam hasa wasomi wa vyuo vikuu walijitokeza kupinga urasmi huu wa kiumbo na kujitokeza na maumbo mbalimbali, mengine ya kiajabu ajabu. Hivyo kuanzia 1968 (yaani miaka michache baada ya mataifa ya Afrika Mashariki kujinyakulia uhuru) mgogoro katika umbo la ushairi umekwezwa hadi leo na unaendelea kuwa na athari na taathira kubwa katika fani ya ushairi na fasihi kiujumla. Mwendelezo wa maumbo ya kisasa umekuwa swala nyeti na la ubishi miongoni mwa wanautamaduni wahifadhina wa kivina na wanausasa ambapo kila mtaalamu anamshutumu mwenzake. Kwa upande mmoja washairi wa kisasa wamestaajabia uhifadhina wa wanamapokeo katika kushikilia umbo la kale na hivyo kuonyesha kuwa umbo huru litaokoa ushairi asemavyo Kahigi na Mulokozi (1973:vi) kuwa:

> ...utunzi wa mashairi hauna budi kuwa na uhai kama ilivyo lugha yenyewe ya Kiswahili; yaani utunzi wa mashairi hauna budi kubadilika. Njia nyingine nzuri hazina budi kuvumbuliwa na watunzi wenye ari ya kuendeleza kipawa chao cha mashairi na lugha ya Kiswahili.

Kijumla mabadiliko haya yalianza kutokea katika tungo za Euphrase Kezilahabi, Ebrahim Hussein, Mugyabuso Mulokozi na Kulikoyela Kahigi ambao waliandika tungo zisizofuata vina na mizani na kuziita mashairi ya kisasa; wengine wanayaita mashairi huru, masivina, mashairi ya kimapinduzi au mapingiti (Njogu na Chimerah 1999:112). Nchini Kenya kuliibuka washairi kama vile Alamin Mazrui, na swala hili limefikia kilele kwa ushairi wa Kithaka wa Mberia. Washairi hawa wakiongozwa na kazi ya Kezilahabi katika Kichomi (1974) na Mashairi ya Kisasa yaliyoandikwa na Kahigi na Mulokozi (1973) walianzisha mwenendo mpya wa ushairi huru ambao uliasi kabisa mpangilio na utaratibu wa arudhi za kale. Hawa wameendeleza kampeni kali na madhubuti kwa kuwahimiza washairi wengine wafuate mtindo huo na kuendelea kufikiria juu ya mitindo mingine wanavyosema Mulokozi na Kahigi (1973:vi):

> Ni matumaini yetu kwamba watunzi wengi wataiga mfano wetu wa kujaribu kuvumbua mitindo mingine; kwani tunaamini kuwa tukishikilia tabia ya kutoibadili mitindo ya Kiswahili, tutawafanya waandishi chipukizi hasa wale wa bara, waamini kuwa sanaa ya ushairi ni ngumu sana au inayohitaji kipawa cha pekee mno au kwamba sanaa hii ni ya watu wa pwani na wenye asili ya Kiarabu na uhusiano na dini ya Kiislamu.

Mwamko huu mpya katika swala la mabadiliko katika umbo la ushairi wa Kiswahili limekuwa changamano na changamoto kiasi cha wahakiki kukanganyika kuelezea ikiwa huu ni ushairi au nathari fupi zenye kutumia lugha ya mkato. Swala hili limeelekea kutoweza kuainisha maumbo au mitungo fulani kama ni ushairi au kitu kingine. Umbo la kisasa katika ushairi limekuwa dhahiri sana kiasi cha kuzua mvutano mkali hasa kuhusu:

[4] K. A. Abedi (1954:28-32) aeleza kwamba mashairi ya mishororo mitatu huitwa tathlitha, mitano huitwa takhmisa, na minne huitwa tarbia. Pia aeleza kwamba utenzi ni ushairi wenye mizani chache kuliko kumi na mbili.

- Fasili ya ushairi
- Tofauti iliyopo kati ya ushairi na kazi nyingine
- Umbo au muundo wa ushairi

Katika mvutano huo wanamapinduzi nao wametoa kijelezi chao kinachofasili ushairi. Kwa mfano Kezilahabi (1976) anatuambia kwamba:

> Ushairi ni tukio, hali au wazo ambalo limeonyeshwa kutokana na upangaji mzuri wa maneno fasaha yenye mizani kwa kifupi, ili kuonyesha ukweli fulani wa maisha.

Ufasiri wa ndani wa fasili hii unatuchochea kuulizia maswali kadha wa kadha mathalani; Kezilahabi anamaanisha nini anapozungumzia juu ya mizani fupi fupi? Je nini kipimo cha ama urefu au ufupi wa mizani? Kulingana na tahakiki ya Mulokozi na Kahigi si lazima ushairi ueleze ukweli wa maisha, nataraji hii inatokana na sababu kwamba ushairi ni sanaa bunifu ya kifasihi ambayo ina uhuru wake wa maudhui. Hapo hapo Mulokozi na Kahigi (1979:25) wanapendekeza fasili ifuatayo:

> Ushairi ni sanaa inayopambanuliwa kwa mpangilio maalum wa maneno fasaha yenye muwala, kwa lugha ya mkato, picha, au sitiara, au ishara, katika usemi, maandishi, au mahadhi ya wimbo, ili kuelekeza wazo au mawazo, kufunza au kueleza tukio au hisi fulani kuhusu maisha au mazingira ya binadamu, kwa njia inayogusa moyo.

Kezilahabi na wenzake waliwachochea na kuwatia shime washairi wengine anavyokiri Alamin Mazrui (1988:vii) katika utangulizi wake wa mkusanyiko wa mashairi yake “Chembe Cha Moyo”:

> Muundo wa mashairi mengi yaliyomo katika mkusanyiko huu umetoka katika mipaka ya ule muundo tuliouzoea na tulioupokea kutoka kwa wahenga wetu kwa kuwa haufuati kanuni za arudhi yaani kanuni za vina, vituo na mizani. Lakini muundo wa aina hii haukuanza na mkusanyiko huu; kuna watu kama Ebrahim Hussein, E. Kezilahabi, Kahigi na Mulokozi na wengineo ambao wametangulia kuutumia katika ushairi wao.

Kwa kufuatiliza na kusisitiza msimamo wake Alamin Mazrui anaanza kwa kutupa shairi “Niguse” katika “Chembe Cha Moyo” (1988:1) lililo na umbo la kipekee:

Nitokapo kizuizini
Nitamwomba yoyote mwendani
        Aniguse
                Taratibu
                polepole
                        Lakini
                        Kwa yakini!
Niguse tena
Unijuze tena
Unifunze tena
        maisha yalivyo
        maisha yaonjavyo
                        ladha yake ilivyo

Nipo hapa nimekukabili
Niguse tena tafadhali!
Niguse!
Niguse!

Umbo hili linamwelekeza msomi katika mwendo wa huruma na hisani. Umbo hili la Mazrui linaambatana na msingi wa fikra za wanamapinduzi za kusisitiza umuhimu wa maudhui katika shairi dhidi ya umbo. Kwamba hisia, ilhamu, taswira na maono ndivyo vitu muhimu katika ushairi. Linahimiza kituo na kitivo cha hisia za mwandishi kiwe katika kiwango cha juu na kuacha wasomi wakiwa na hamu ya kutaka kuuendelea kuusoma utungo huo. Katika mkururo huo, Mazrui anaendelea kuzua maumbo mengineyo kwa mfano shairi “Damu ya Harara” (uk. 16):

Roho isoburudika
    ila kwa fazaa ya moto
                moto wa mapinduzi

Yaja kujitosa
    katika mkonde wa moto
                moto wa ukombozi

Roho yaja ... kwa sauti ya haki
                yenye maumivu
    na hukumu ya dhiki
                yenye maangavu

Si kwamba washairi wa kimapinduzi walikataa kata kata vipengee vya kimsingi vya ushairi wa kimapokeo bali inavyobainika ni kwamba wakati mwengine wanavihifadhi lakini kwa mitindo mingineyo. Kwa mfano muundo wa mizani 8/8 katika kila mshororo na idadi ya mizani 64 kijumla katika kila mshororo sasa unaweza kuwa na hiyo idadi ya mizani 8 lakini katika mshororo mmoja na nane katika mshororo unaofuatia lakini ukitazama kwa makini utagundua kwamba hivi vipande viwili vikiunganishwa vinaweza kuunda mshororo mmoja kwani utapata kwamba mshairi huanza mshororo unaofuata kwa herufi ndogo. Kwa upande mwengine utapata kwamba mshororo wa kwanza una kina kinachofanana na kile cha mishororo ya tatu, nne na sita. Katika umakinifu huo mshororo wa pili unaweza kuunganishwa na mshororo wa kwanza na kuwa mshororo mmoja, wa tatu ukaunganishwa na wa nne, wa tano na wa sita na wa saba na wa nane na hivyo kurejelea mistari minne kama katika tarbia yenye kina cha kati na cha nje. Tazama mfano ufuatao wa shairi “Chuo” la Mazrui (uk 2).

| *Muundo wa Alamin* | | *Muundo wa kimapokeo* | |
|---|---|---|---|
| Nilisozwa na mawimbi | (8) | ............8.......... mbi | ............8.......... di |
| kapinduka gudi gudi | (8) | ............8.......... mbi | ............8.......... di |
| Bahari ikanidhambi | (8) | ............8.......... mbi | ............8.......... di |
| kanitokoma baidi | (8) | ............8.......... zi | ............8.......... a |
| Kaomba yangu maombi | (8) | | |
| tamaa ikanidhidi | (8) | | |
| Chuo cha ukombozi | (7) | | |
| kikaja kunikomboa | (8) | | |

Shairi hili linatuthibitishia ya kwamba washairi wa kimapinduzi wana uwezo wa kutunga mashairi kwa uzingatifu wa arudhi zilizopo ila tu wameasi kaida hii kimaksudi. Wanavyojitetea ni kwamba fikra za kuwa wao hawazimudu mbinu za ushairi na kwa hivyo wameshindwa kutunga mashairi ni hoja ya taasubi tu. Kwao matumizi ya lugha, jazanda na taswira inadhihirisha kiwango cha juu katika utunzi wa mashairi.

Mtaalam Said Ahmed Mohamed hakubaki nyuma katika mgogoro huu na katika shairi “Nawaita Washairi” kwenye “Sikate Tamaa” (1980:3) msanii huyu anasisitiza ari yake kwa kusema:

Nawaita washairi, tukutanishe mikono
Katika hii safari, iliyo na mapambano
Tuacheni kuhubiri, pia mengi mashidano
    Tuandikeni kwa ari

Tubadilishe mitindo, katika wema wiano
Tuyafichue mavundo, tuonyeshe migongano
Tushikilie upendo, umma wenye msongano
    Tuandikeni kwa ari

Said Ahmed Mohamed mwenyewe anajihisi kwamba amebadilika kifani kutokana na ushawishi wa hisia za miundo na mitindo mbalimbali. Kwake ushairi si vina na mizani tu, na

wala si uhuru tu. Ni uhuru wa busara unaoshikana na hisia na ufundi wa utunzi. Kwa ukakamavu na uthabiti, katika shairi “Arudhi” kwenye “Jicho la Ndani” (2001:78) anasema:

Kina, cha nini kina?
Kina, sikitaki kina – iwapo chalazimishwa:
    La kije kwa hiari
    Tena kije vizuri
    Kilingane na pumzi
Zitazonifanya kuzamia kwenye vina na kuogelea!

Mizani, kwa nini mizani?
Mizani, sitaki mizani – iwapo sina cha kupimia
    Ila kwa mazito mawazo
    Un’elemee mzomzo
    Unijie kwa dhamiri
Itakayonipelekea, kutingisha sawiya maudhui na fani!

Urari, wa nini urari?
Urari, sitaki urari – iwapo ni wa kubambia
    Ila uje kwenye mistari
    Uchukue takriri
    Uoane na hisia
Zitakazoumua umbo lis’o mshazari

Ubeti, kwa nini ubeti?
Ubeti, sitaki ubeti – iwapo utashurutishwa:
    Ila ujenge nudhumu ya hiari
    Ing’ae kama johari
    Imara il’osadifia
Itakayoimbika, kwa ari kutoka kila ubeti!

Muwala, kwa nini muwala?
Muwala, sitaki muwala – iwapo hauji kwa wenyewe
    Ila uje kwa lazima
    Kwa kariha il’o njema
    Inivae, inikae kwa hamu
Itakayofanya: muwala utiririke hadi hatima!

Baada ya ukakamavu huo wa kutokubali kulazimisha matumizi ya vina, mizani, beti na muwala, mshairi anaendelea kushutumu umbo hilo la awali kwa kutuchorea taswira ya umbo lingine katika shairi “Walipopapasa Walipo” (uk.72):

Ubeti wa kwanza:

Lipopapasa walipo wakaona 'metuwaa
Wakagundua vipapo vina kwao vinang'aa
Wakang'ang'ania papo pengine hapakufaa
Hapo wakakoma
Hapo wakasema
Ushairi umekaa!

Shairi hili lina beti nne na linafululiza muundo huu huu katika beti zote. Kimaudhui shairi hili linawakebehi wanamapokeo kwa kufikiria kuwa utunzi wa vina, muwala na mizani ndiyo upeo wa ushairi. Anavyoelezea Said Ahmed Mohamed fani na miundo ya mengi ya mashairi katika "Jicho la Ndani" imeathiriwa sana na yale ambayo yamekuwa yakijiri katika jamii zetu na hasa hali ya wakati huu anayoita "uhalisiamazingaombwe"; hali ya ndoto si ndoto, ukweli si ukweli (Mohamed 2002:ix).

Nionapo mimi kilele cha mazingaombwe haya ya mabadiliko ya kimuundo kimefikia upeo katika ushairi picha au umbo halisi katika ushairi wa Kithaka wa Mberia kwenye diwani ya "Mchezo wa Karata" (1997). Uvumbuzi wa haya mashairi picha au halisi umewashangaza wasomi wengi nchini Kenya. Ushairi huu umeumba upeo mpya wa mtazamo wa ushairi na kujitokeza kwa umbo la kiupekee ambalo limezua changamoto kwa wahakiki na wachambuzi wa mashairi. Kwa mfano shairi "boga" linalochukua umbo la duara (uk. 2-3):

mboga si
uliozaa urithi
mboga wangu,
hili, ni
hukuupanda urithi
sikuupanda wetu;
tulipozaliwa boga
tuliukuta hili
unastawi basi,
shambani, si
shamba mali
tulililoachiwa yako
na si
wazazi; mali
maadamu yangu
sisi ni
wawili, mali
tu yetu;
warithi basi
wa nasisitiza,
shamba tulikate
hili, sehemu
utajiri mbili,
uliomo sehemu
shambani, sawa
si yako
urithi na
wako yangu

Kithaka wa Mberia ameendeleza hali hii kwa kutuumbia tena shairi la “Nyumba” (uk. 17) amabalo linachukua hasa muundo wa kijibanda na shairi la “Dau Haliendi” (uk. 32) ambalo linatupa nusu duara:

*Nyumba*

nyumba
hii ambayo
ilifumbwa kwa
mawe yaliyoumbwa
na maumbile,
mawe ambayo
yalisongwa na
maskini, nyumba
hii ambayo
ilisimamishwa kwa
saruji itokanayo
na viungo
vya ardhi vilivyochimbwa na
yahe, nyumba
hii iliyoezekwa
vigae vitokanavyo
na udongo
kimano tuliourithi
kutoka mama,
nyumba hii
iliyopambwa kwa vioo vilivyotengenezwa
na matambara, kwa nini wasistarehe katika nyumba
hii wale ambao misuli yao iliipa uhai?

*Dau Haliendi*

ingawa
limo
mbioni,

hili
dau
la
kusafi
mamilioni,
haliendi;
huu
ni
mwendo
duara-
unaduru,
ni
mwendo
mzunguko-
unazunguka
mwendo
mpeto-
uaopeta,
hauwi
safari,
bali
hupambazika
mamilion
kwamba
wanasafiri
katika
bahari
ya miaka

Maumbo haya ya kimazingaombwe[5] yanazidi kuendelezwa na mwandishi katika diwani ya "Bara Jingine" (2001) katika shairi "Mruko wa Nyuki" (uk. 20-25). Katika mtungo huu tunakumbana na nyuki wa Afrika ambao utulivu wao ulisambaratishwa na wageni. Na hapo wakaanza safari ya kutafuta tiba. Katika safari yao walifika njia panda ambapo wengine walifuata kushoto na wengine kulia. Baada ya kitambo njia ya kushoto iliporomoka. (Wazo hili la kuporomoka kwa njia linaonyeshwa moja kwa moja kwa matumizi ya mistari ya

[5] Miundo hii inarejelewa kuwa ya kimazingaombwe kwa vile imekiuka mipaka ya uhalisi wa umbo la mashairi. Kweli ni miundo ya kuajabia ambayo ina upekee wake usiyoweza kulinganishwa na miundo mingineyo ya ushairi duniani.

mishazari kwenye mchoro huu). Baadaye waliobaki wakajiunga na wengine katika njia ya mkono wa kulia.

*Mruko wa Nyuki*

| | | | |
|---|---|---|---|
| tutasema | ambayo | | njia |
| lini | haikutufaidi | | moja |
| baada | tulichoka | iliingia | kulia |
| ya | nyoyo | nyingine | ikapitia |
| amani | joto | kushoto, | baadhi |
| yetu | La | yetu | tulisafiri |
| kuvurugwa | dhiki | kushoto, | wengine |
| Na | likatukausha | walifuata | kulia |
| wageni | stahamala | baada | ya |
| sisi | tulikalamua | kitambo, | ghafla |
| nyuki | akili | njia | ya |
| wa | zikajiri | kushoto | |
| afrika | ndoto | i po | |
| tulipitia | ndoto | li ro ka | |
| nyanda | jamala | mo | |
| tata | ndoto | walikuwemo | wakajiunga |
| nyanda | za | | na |
| zenye | tiba | | njia |
| walembe | tulikakamua | | ya |
| tuliloa | mabawa | | kulia |
| machovu | mabawa | | pamoja |
| machovu | safari | | ka |
| | | | |
| ya | safari | | nguvu |
| ukusanyaji | ya | | za |
| ukusanyaji | tiba | | misuli |
| wa | ulianza | | tulijizati |
| mbelewele | mwendo | | ti |
| viungo | mwendo | | na |
| vya | wa | | kuufikia |
| kutengeneza | mabawa | | mti |
| asali | na | | wa |
| | nyoyo | | |

*hii ni sehemu tu ya utungo huu, sikunukuu utungo wote.

**Athari za maumbo mapya katika uhakiki na uchambuzi wa Ushairi**

Hapana shaka kuwa miundo hii mipya ni mabadiliko makubwa katika ushairi wa Kiswahili na hivyo kuandikisha historia mpya katika ushairi. Ilhamu ya Kithaka wa Mberia ya kuwasilisha mawazo ya ndani kwa matumizi ya picha halisi ili kudhihirisha uwazi wa ayatamkayo, si tu maono mapya katika uvumbuzi wa usanii kisayansi bali pia uvumbuzi wa falsafa mpya ya

kisanaa. Kwa kweli ushairi huu umedidimiza matumaini ya kuhifadhiwa kwa kanuni za kiarudhi za ushairi jadi na kwa miaka ijayo huenda vizazi vya kesho kutotambua uwepo wa arudhi hizi katika ushairi jadi. Kwa sasa tunaweza kuzungumzia juu ya maumbo mbalimbali ya ushairi wa Kiswahili yakiwemo duara, nusu duara, nyumba n.k. Ikiwa tutakubaliana kwamba haya ni maendeleo katika umbo la ushairi, basi tunaweza kusema kwamba ushairi huru umefufua na kuzindua talanta mpya ambazo pengine hazingejidhihirisha ikiwa wanausasa hawangejitokeza waziwazi.

Hata hivyo maumbo haya mapya ya Kithaka wa Mberia yanazua athari nyingine katika uhakiki na uchambuzi wa ushairi. Tumesema kuwa maumbo haya yanadhihirisha uwazi wa ayasemayo mtunzi na hivyo basi tunajiuliza kwamba ikiwa mtunzi atadhihirisha taswira ya maudhui yake, je mhakiki atafanya kazi gani na ilhali mtunzi ashamdokezea yote. Ubora wa ushairi hutokana na uchangamano wa ufasiri wa maudhui yake yanayotokana na taswira anazoziumba mhakiki na kumwongoza katika kufikia ufasiri mwafaka. Mtunzi anafanya ufasiri wa maudhui kutokuwa changamano na hivyo kutozua changamoto za kiusomi. Kwa mfano linganisha shairi “Boga” (Mberia 1997:2-3) na shairi “Mnazi Vuta Nkuvute” (Abdilatif 1973:17-22). Katika ngonjera hii mhakiki anaumba taswira ya watu wawili ambapo Badi amekwea mnazi na kuukatalia na Ali amenyimwa nafasi ya kukwea huo mnazi. Ingawaje katika mashairi yote mawili picha tunayoipata inahusu kunyanyaswa kwa kunyimwa haki, umbo la boga ni wazi zaidi kuliko taswira za mnazi ambapo mhakiki lazima atumie kitivo chake cha busara katika kufichuwa siri iliyopo. Linganisha pia na shairi “Mruko wa Nyuki” (hapo juu). Kuna hatari katika kuonyesha uwazi katika fasihi kwa sababu ufiche ni kipengee muhimu sana katika fasihi na humpa mhakiki nafasi ya kudadisi dadasi yaliyomo kwa mamlaka ya hekima zake. Kwa hivyo tunabaki kujiuliza je usanii uko wapi katika kazi kama hizi.

Wanamapinduzi wenyewe wanasema kuwa ushairi wa kisasa umetumia lugha sanifu na isiyochangamano ili ujumbe ufikie uma wote. Ni muhimu kutaja kwamba lugha ya kifasihi na hasa lugha ya ushairi ni lugha maalum ambayo haiwezi kuchukuliwa kijuu na msanii yeyote kwa vile ina lengo kuu katika kuumba umbo thabiti la shairi, ndiposa kipengee hiki kinabakia kuwa kiungo muhimu cha kutambulisha ufasihi wa kishairi wasemavyo Mulokozi na Kahigi (1983:25):

> Ushairi lazima uguse hisi, lazima umsisimue anayeusema, kuusoma na kuuimba na yule ausikilizae. Shairi lisilogusa hisi ni kavu na butu, hata kama limesafiriwa katika vina na urari wa mizani, shairi hilo litaishia katika kuhubiri tu.

Washairi huru wanaonelea kwamba ushairi awali ni mgumu kwa kutumia mafumbo magumu na lugha ya kale hasa wakati ambapo waandishi wananga'ngania kutosheleza sheria za utunzi, hivyo basi ujumbe katika ushairi huu haumfikii mwananchi wa kawaida ambaye huhofia kusoma mashairi kwa sababu ya uchangamano wake wa kuwasiliana. Fikra zilizopo ni kwamba ushairi huru umepanua uwanja wa hadhira kwa sababu ya lugha yake ya kawaida ambayo inawafikia hata watu ambao hawana talanta ya kubuni, kuimba wala kuhakiki ushairi. Hivyo umbo hili jipya limewavutia sana watunzi na wahakiki na kuongezea idadi ya watunzi wa mashairi kwa sababu ni:

- Rahisi
- Huwasilisha mawazo kihuru
- Huu ndio usomi

Baadhi ya mashairi awali yawe ya maudhui ya kilimwengu au kidini yaliimbwa na manju katika sherehe mbalimbali za unyago, jando, matanga, harusi na burudani mbalimbali, madrasa na katika mikusanyiko mingineyo ya kidini. Ingawaje hakukuwa na sauti maalum iliyofaa uimbaji huu, washairi wana uhuru wa kuimba mashari haya kwa mahadhi na laani wazichaguwazo mradi tu yanachukuana na mtiririko wa mtungo. Tungo hizo zilikuwa na uzito wa mawazo maadilifu na mizani ya sauti kulingana na lahani zilizowavutia wasikilizaji. Mtiririko wa vina, mizani, takriri na ulinganifu wa mishororo ni vipengee muhimu vinavyosaidia kuimbika kwa ushairi huu. Ukamilifu huu wa ushairi uliwafanya watunzi awali kusisitiza kuwa shairi lazima liimbike yaani "ushairi ni wimbo"[6]. Hata hivyo mabadiliko yaliyopo ni kuwa wingi wa mashairi ya leo hayaimbiki kwa vile hayakunuiwa mwanzo kuimbwa katika sherehe maalum. Uwanja wa ushairi umepanuka na kubadilika pia. Mashairi yaandikwa kwa minajili ya kusomwa darasani, kuchambuliwa na kuhakikiwa katika madaraja ya juu ya kiusomi.

Ingawaje tumeshuhudia tafsiri ya mashairi kutoka Kiarabu hadi Kiswahili kwa uhifadhi wa vina na mizani, mashairi huru yanaweza kutafsiriwa bila wasiwasi wowote kwa vile mtafsiri hafungwi tena na utaratibu wa arudhi hizi; alivyofanya Kezilahabi katika ushairi wa "Kichomi". Kupitia mbinu hii sanaa ya Ushairi wa Kiswahili imesambazwa kote na kusomwa na wengi. Kwa sasa mtafsiri na mfasiri ana uhuru mwingi wa kuchezea lugha ya mtunzi awali na pia kuongezea maneno na mawazo yake mradi amehifadhi ujumbe awali.

## 3. Hatima ya Ushairi wa Kiswahili

Katika mitazamo na mabishano haya yote ni muhimu kujiuliza swala la ni ipi hatima ya ushairi wa Kiswahili kiumbo. Nini ambacho tutarithisha kizazi kijacho kwa misingi ya kuendeleza sanaa hii yenye utata mwingi? Tusipolifikiria kwa makini swala hili basi tutabakia pale pale katika utangulizi wetu kwa maoni ya mtaalamu Heidegger kwamba je sisi ni

[6] Katika fasili yake Shabaan Robert alisema kwamba "wimbo ni shairi ndogo na shairi ni wimbo mkubwa" na "utenzi ni upeo wa ushairi" (Massamba 1983:55).

wafikiriaji washairi au washairi wafikiriaji. Hili ni swala changamoto ambalo lazima likabiliwe sasa ikiwa twataka kupata mwelekeo wa ni wapi ushairi wendapo. Wote washairi wa kimapokeo na wanausasa wafaa kujisahili ikiwa wametimiliza malengo yao na kujiuliza ni hatua gani uvumbuzi huu umeleta katika kustawisha na kuendeleza ushairi wa Kiswahili. Ni dhahiri kwamba sanaa imo katika kinyanganyiro cha soko na ni vema kujiuliza ikiwa sanaa ya ushairi inabishana vema katika soko la uwanja wa sanaa ulimwenguni. La sivyo wapenzi wa sanaa hii wana malengo gani ya kuiinua fani hii ili ifikie kiwango hitajika. Tupende tusipende, utunzi wowote ule ama unadunisha au kudumisha utanzu huu wa fasihi. Swala kuu ambalo yafaa zote wapenzi wa ushairi tujiulize ni je tunahitaji kizazi chetu cha baadaye kirithi nini; mkorogano wa maneno au mtindo na muundo wenye utaratibu maalum wanavyohofia wataalamu mbalimbali. Kuhusu swala hili la hatima ya ushairi wa Kiswahili, S. Chiraghdini akimwandikia Ahmad Nassir utangulizi wa “Malenga wa Mvita” (1971:14) anateta:

> Kwa Kiswahili, tungo zifuatazo mwendo huo, mizani zake hazitakuwa na kichwa wala miguu, kanuni zote za ushairi wa Kiswahili zitakuwa pindu, vina vitakuwa havijulikani mwanzo havijulikani mwisho na lugha yenyewe itakuwa chapwa au kuzidi. Na tungo hizi zikikubaliwa kuwa ni mashairi basi ushairi wa Kiswahili utakuwa umeanguka kitakotako.

Hii ndiyo wasiwasi aliyokuwa nayo K. Amri Abedi na kumwelekeza kutunga sheria za utunzi wa mashairi. Ingawaje Abedi alitunga sheria hizi mwaka wa 1954, tayari alianza kulalamika kuwa mengi katika mashairi yanayotungwa siku hizi yanaelekea kupunguza thamani ya mashairi ya Kiswahili mbele ya lugha nyingine[7]. Wafuasi wengine wa ushairi jadi, wanayaunga maoni haya mkono kwa kuonelea kuwa ushairi umekosa mwelekeo na kwamba kwa kuendeleza maumbo haya mapya ladha ya ushairi inapotea na hatimaye utanzu wa ushairi utatoweka na kitakachotokea ni utanzu wa nathari unaotumia lugha kwa ufupi. Kwa mfano akinukuliwa na Wallah Bin Wallah (1988:xv) Mwalimu Hassan Mbega analalamika kuwa mashairi ya siku hizi hayana ladha, ufundi na mwelekeo imara asemavyo:

> Ingawa watunzi ni wengi sana sasa lakini mashairi mengi si mazuri ya sifa ya ushairi, kadhalika daraja zote za utunzi zimetupwa na kushikiliwa daraja moja tu. Pia lugha ya kishairi sio itumiwayo na wengi wa watunzi wa leo. Jambo hilo ingawa halichunguzwi na washairi, labda kwa kutofahamu kuna hasara kubwa ambayo imeufanya ushairi wa sasa wa Kiswahili usiwe wa thamani na umedharauliwa sana.

Kwamba jambo litakaloridhishwa kizazi kijacho ni kivuli au tuseme taswira na ishara ya ushairi inavyoelezwa katika “Ushairi ni sanaa” (Wallah 1988:151):

Ubeti 2 Hawasani huharibu, tungo sizo kama hizi
Hata siko kujaribu, bali ni ung’anganizi
Kazi mbovu ni harabu, hazifaidi vizazi
Watungao siku hizi, si watunzi wa kutibu

[7] Abedi katika utangulizi wa diwani yake anaeleza kwamba amesoma mashairi katika lugha ya Kiingereza, Kiurdu, Kiarabu na Kiajemi. Anafahamu namna ambavyo watu wa mataifa mengine wanavyokusanya fikra na kuzipanga. Mitindo hii si mbali na utunzi wa zamani na wa kipindi chake.

Ubeti 5 Si lolote hughilibu, hawana jema pambizi
Mizani wanaharibu, kwa maneno ya gegezi
Na vina hawaratibu, beti zina uchafuzi
Watungao siku hizi, mwawaonaje mababu?

Ubeti 6 Mwawaonaje mababu, ati hawa ndo wajuzi
Waliozuka karibu, na nudhumu za uchizi
Zisofata taratibu, za kunga na utondozi
Watungao siku hizi, ni watunzi wa lakabu

Wallah Bin Wallah azidi kuwahimiza washairi kutunga ushairi kwa utaratibu maalum katika shairi “Kufu ya Umalenga” (Wallah 1988:156):

Ubeti 1 Tunu hii ya johari, mwatunzaje umalenga?
Masombo nimejifunga, kusawiri mistari
Mistari ya kutunga, nudhumu za umahiri
Nami nilunge wahenga, makungwi wa ushairi

Ubeti 3 Tunu hii ya johari, mwatunzaje umalenga?
Miiko yakwe nachunga, nisiende mashazari
Mizani vina hapanga, kwa idadi ya fahari
Beti nazo haziunga, kwa muwala wa nadhari

Ubeti 7 Tunu hii ya johari, mwatunzaje umalenga?
Kaida sipigi chenga, chambueni mtakiri
Ningawa mbuji mchanga, tungo njema nahitari
Sipendi kuvungavunga, amali ya uayari

Wanamapokeo wanapoendeleza wasiwasi wao huu wanamapinduzi wana uhakika kuwa upotevu wa vina na mizani katika ushairi si jambo la kutilia hofu juu ya hatima ya ushairi. Kwamba mienendo mipya ya kisasa inahuisha na kuusukuma mbele ushairi. Ushairi huru badala ya kuangusha ushairi wa Kiswahili, utapanua, kuusambaza na kuuimarisha. Uhakiki na utunzi wa ushairi utawavutia wengi ambao walihofia ugumu na ukale wa maumbo awali na hivyo taaluma hii kuendelezwa na wadogo kwa wakubwa, wataalamu kwa watu wa kawaida.

Wakati huu tunapata kwamba watunzi wa tungo za kiarudhi sasa ni haba kwa vile wengine wamevuka sakafu kuungana na wanamapinduzi ilhali wengine hawajui waegemee wapi. Kwa mfano itakumbukwa kwamba miongoni mwa wataalamu wachache tulionukuu fasili zao, Abdilatif Abdalla anajitokeza katika kundi la wanamapokeo, lakini anapomwandikia Said Ahmed Mohamed utangulizi wa “Sikate Tamaa” (1980) anampongeza kwa ujasiri alioufanya katika kubadilisha miundo ya ushairi soelevu. Anaonyesha kwamba umbo la shairi lina nafasi kubwa sana ya kuweza kuvyaziwa miundo kadha wa kadha na ni matumaini ya Abdilatif Abdalla kuwa watakaomfuata Said Ahmed Mohamed watatambaa na kuendelea kuikuza sanaa hii. Haya yametekelezwa na washairi wa kisasa na huenda mtindo ukawa ni huo huo siku za usoni.

Nilipotanguliza awali, mikondo ya ushairi wa kisasa imevamiwa na wasomi, la ajabu ni kwamba tumeanza kuona kwamba talanta hii adimu imetoka mikononi mwa wazee wenye hekima na busara zao kule kijijini na kuwa mali na zao la maprofesa wa vyuo vikuu. Kwa urazini wao wasomi hawa wanatilia shaka uwasilishaji huru wa ujumbe kwa umma kupitia ushairi jadi. Ni kana kwamba mbinu hifadhina za ushairi wa kimapokeo ni kizuizi cha kuwasilisha maudhui ya kisasa ya kiukombozi. Mtunzi Wallah Bin Wallah (1988:viii) anaendeleza wasiwasi hiyo anaposema:

> Wahenga walisema wengi wape. Usipowapa watachukua kwa mikono yao. Maadam idadi ya wasomi inazidi kuongezeka, nachelea kwamba asaa siku moja watatumia wingi wa mikono yao kunyakua kanuni za sanaa ya ushairi na kuzitupa katika bahari ya sahau.

Wanamapokeo wazidi kusikitika kwamba miundo ya kisasa ikiendelea kukubalika ushairi unadidimia na mwishowe utakufa. Haya ni madai mazito sana ambayo ni lazima tuyatafutie suluhisho ikiwa tunataka kuendeleza na kukuza sanaa hii.

Ushairi umekuwa chombo maalum chenye nguvu na uwezo wa kutumiwa na wasomi katika kupigania haki za kijamii na kisiasa inavyojitokeza katika ushairi wa Shaaban Robert, Abdilatif Abdalla, Kithaka wa Mberia, Alamin Mazrui, Said Ahmed Mohamed na wengineo. Mbinu zitumiwazo sasa hivi ni nyumbufu na huweza kukabiliana vema na mawazo mageni hata kama ni kutohoa au kuwasilisha wazo kwa lugha ile ile ya awali. Kwambatana na haya mbinu nyinginezo za kiisimu katika ushairi: fonolojia, mofolojia, sintaksi na semantiki sasa ni nyumbufu zaidi na washairi wanaweza kuchezea chezea vipengee hivi vya lugha ili kuzua maumbo mbali mbali wayapendayo. Maumbo haya yamerahisisha sanaa ya utunzi wa ushairi.

Nakubaliana na kutokubaliana na Wallah Bin Wallah katika maoni yake kuwa licha ya kupotea kwetu[8] tumefikia kiwango ambacho lazima tujitafute tujijue tulipo. Anaona kwamba tumekuwa wakatili na wauaji wa mila na desturi zetu kwa kuamini na kuthamini mambo ya kizungu bila kudadisi kwanza. Kwamba kumetokea miigo ya papara. Sikubaliani naye anaposema kuwa “maendeleo maana yake si kuleta sura mpya bali ni kusonga mbele kwa kuleta mabadiliko yenye tija ya kuinua hali katika maisha ya jamii”. Kwa kweli mitazamo ya dhana ya maendeleo ni tofauti kutoka binadamu mmoja hadi mwengine, na ni dhahiri kwamba kubadili umbo la kitu wafanyavyo wasanii wa uchongaji na uchoraji katika kunakisisha kazi zao ni hatua ya kimaendeleo na ndiyo mkondo waliouchukuwa washairi.

Kwa namna nyingine ubishi na upinzani uliopo kati ya wanajadi na wanausasa umezidisha ujeuri miongoni mwa watunzi kiasi cha watu kutunga chochote na kudai kwamba hilo ni shairi, kwa kisingizio cha maendeleo au tuseme mabadiliko katika utamaduni wa kijamii. Tujuavyo ni kwamba maendeleo ni kupiga hatua kwa kuleta hali bora kiuchumi, kielimu, kisiasa, kiufundi, kiutamaduni, kiusanii, kimaisha na kijamii. Hatukatai ushairi wa kimapinduzi umepiga hatua kimaendeleo lakini lazima kuwepo utaratibu bora wa kiusanii ambao utaelekeza watunzi wa mbeleni. Kwa kweli upotoshi wa sanaa ya ushairi hautaleta

[8] Wallah Bin Wallah aonelea kuwa kwa kuacha utunzi wa kijadi, washairi wamepotoka na kupotea na hivyo anahimiza kwamba “jungu kuu halikosi ukoka”.

maendeleo yoyote, bali utata katika kufasili dhana ya ushairi itakwezwa na wahakiki hawatawahi kupata fasili mwafaka kwa utanzu huu. Hivyo basi hadhi, heshima, taadhima na utukufu wa ushairi utashushwa. Ushairi hautavutia na kupendwa na wengi inavyotarajiwa.

## Tamati

Mivutano na ubishi katika maswala ya kiumbo na kimuundo yameipa hadhi ushairi wa Kiswahili miongoni mwa mashairi mengineyo ulimwenguni na miongoni mwa tanzu nyinginezo. Tuzingatie kwamba siku hizi kuenea kwa vitabu, magazeti, majarida na mtandao kumesambaza utunzi wa ushairi kote ulimwenguni. Swala la umbo la ushairi wa Kiswahili limekuwa maarufu katika taasisi mbalimbali za kiusomi hasa vyuo vikuu. Maadam umbo jipya limeupa ushairi wa Kiswahili ubishani mkali kwa umbo la awali na kuipa nguvu na "mvuto" zaidi wa kufumbua macho ya wasomi na mitazamo yao kuhusu fasili ya ushairi wa Kiswahili. Umbo hili limewazuzua na kuwachochea hata wale waandishi wa umbo la zamani ambao wameungana katika kuendeleza mitindo hii mipya na pengine wangalifufuka Shabaan Robert na Kaluta Amri Abedi leo hii wangeunga mkono swala hili au kuacha kutunga mashairi.

Ni wazi kwamba wengi wa washairi wa kisasa wametumia elimu na maarifa yao kisawasawa katika kutambua mbinu na mitindo mipya ya usanii. Wangali mbioni kuendelea kusaka na kusakanya mbinu nyingine mwafaka zaidi ili kukabiliana na wakati na mahitaji ya sanaa katika kipindi hiki na kijacho. Uvumbuzi na ufanisi wa maumbo mapya yenye mivuto na amali za kiujumi umewazindua washairi kuanza kupekua pekua na kudadisi undani na uamilifu wa ushairi. Uumbaji upya wa sanaa hii umevuta na kunasa hisia, mawazo, ufahamu na akili za msomaji. Haya yote yamelenga katika kuleta hali bora na mwafaka katika maisha ya kijamii. Tunawahimiza wapenzi wa ushairi waendelea kuibua mbinu mpya ziwe za kiarudhi au taratibu nyinginezo katika kuimarisha utanzu huu.

Wakati tuliomo ni tata na changamano zaidi katika uelekezi wa umbo lifaalo ndiposa tunapata kwamba wahakiki na wachambuzi hasa wanafunzi hukaganyika sana katika kufasili dhana ya ushairi. Wanazidi kuuliza maswala yaso ukomo kuhusu je nini umbo halisi la ushairi wa Kiswahili. Kazi ya fasihi si tu ukusanyaji na mrundiko wa mbinu za kifasihi bali mpangilio na ufinyanzi wa mbinu hizi katika kutupa umbo sahihi la mtungo mzima unaoangazia umuhimu wa kila kipengee kilichomo. Ilivyo wakati huu, hamna umbo mwafaka la ushairi ilivyoonyeshwa katika wasilisho hili. Yafaa washairi wabuni nadharia elekezi ambazo zitawaongoza wahakiki na watunzi wa kazi hii. Ni muhimu kutaja kwamba maumbo yote ya awali au kisasa yana thamani yake ambayo si haki kupuuzwa kwani vipengee vilivyomo kwa maumbo yote vimewezesha tungo hizi kudumu na kusambazwa kwa kipindi kirefu ulimwenguni kote.

Ni matarajio yangu kwamba washairi wakiungana pamoja katika kutafuta umbo teule la ushairi itakuwa maendeleo makubwa sana katika kukuza na kuendeleza fasihi ya Kiswahili. Kwa kweli kipindi chenyewe ni kigumu kwa sababu migogoro na mivutano ingalipo na

hamna yeyote katika mapote haya anayekubaliana na maoni ya mwenzake. Kila pote linadai umaarufu wake kwa kuzidisha chuki na hasira kwa pote pinzani. Bora ni kwamba tungo awali ziendelezwe sambamba na tungo za kisasa kwa minajili ya mlinganuo wa kiusomi. Ni muhimu kuwa tenzi, tumbuizo, tathlitha n.k ziendelee kutungwa. Natumaini wasilisho hili litakuwa changamoto kwa wapenzi wa tungo hizi kuvumbua mitindo mipya ya kuziendeleza walivyofanya Shabaan Robert na wengine enzi zao.

## Marejeo


Abdalla, Abdilatif. 1973. *Sauti ya Dhiki*. Nairobi: Oxford University Press.

Abedi, Kaluta Amri. 1954. *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Heidegger, Martin. 1971. *Poetry, Language, Thought*. New York: Harper & Row Publishers.

Kahigi, Kulikoyela & Mugyabuso M. Mulokozi. 1973. *Mashairi ya Kisasa*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Kahigi, Kulikoyela & Mugyabuso M. Mulokozi. 1979. *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Kezilahabi, Euphrase. 1974. *Kichomi*. Nairobi: Heinemann.

Kitula, King'ei & Amata Kemoli. 2001. *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi: Acacia Stantex Publishers.

Kuvuna, S.M, Mvati, M.N & P.A Maliachi. 1992. *Nuru ya Ushairi: Mwongozo na Uchambuzi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Massamba, David. 1983. Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili. *Fasihi* [Makala za Semina ya Waandishi wa Kiswahili III], imehaririwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Uk. 55-94.

Mayoka, Jumanne M. 1984. *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mazrui, Alamin. 1988. *Chembe Cha Moyo*. Nairobi. Heinemann Kenya Ltd.

Mberia, Kithaka wa. 1990. Umbo La Mashairi. *Mwamko* 5 [Jarida La Chama Cha Kiswahili Chuo Kikuu Cha Nairobi]: Uk. 80-111.

Mberia, Kithaka wa. 1997. *Mchezo wa Karata*. Nairobi: Marimba Publications Ltd.

Mberia, Kithaka wa. 2001. *Bara Jingine*. Nairobi: Marimba Publications Ltd.

Mnyampala, Mathias. 1965. *Diwani ya Mnyampala*. Dar es Salaam: East African Literature Bureau.

Mohamed, Said Ahmed. 1980. *Sikate Tamaa*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mohamed, Said Ahmed. 2002. *Jicho La Ndani*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mwai, Wangari. 1988. New Trends in Ushairi. Tasnifu ya kupata digrii ya uzamili (M.A.) ambayo haijachapishwa. Chuo kikuu cha Nairobi.

Nassir, Ahmed. 1971. *Malenga wa Mvita. Diwani ya Ustadh Bhalo*. Nairobi: Oxford University Press.

Njogu, Kimani & Rocha Chimerah. 1999. *Ufundishaji wa Fasihi. Nadharia na Mbinu*. Nairobi. Jomo Kenyatta.

Wallah, Wallah bin. 1988. *Malenga wa Ziwa Kuu*. Nairobi: East African Education Publishers.